

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegrams "AFYA", DODOMA  
Nambari ya simu: 255-026-2323267/2351196  
Fax Na.255-22-213806



Mji wa Serikali - Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S. L. P 743,  
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI  
KUIONDOA MAABARA YA TAIFA KATIKA JUKUMU LA KUCHUKUA  
SAMPULI ZA WASAFIRI.

Morogoro, Jumamosi Februari 27, 2021.

Maabara ya Taifa imekuwa ikichukua sampuli, ikizichakata na kuzipima, kutoa majibu pamoja na uandaaji wa vyeti kwa wasafiri. Aidha, katika kutekeleza jukumu hilo, Maabara ya Taifa imekuwa na changamoto ya wasafiri wanaofika kuwa wengi hivyo kusababisha msongamano, pamoja na miundombinu ya huduma za maliwato na eneo la maegesho ya magari kuwa finyu.

Wizara ya Afya imeamua kuiondoa Maabara ya Taifa katika chaguo (option) ya kituo cha kutolea sampuli za kupima COVID-19 kwa wasafiri katika mfumo wa kutuma miadi wa [pimacovid.moh.go.tz](http://pimacovid.moh.go.tz) kuanzia tarehe 01 Machi, 2021.

Aidha, utaratibu wa kupima sampuli kwa kipimo cha haraka cha protini za kinga (COVID-19 IgM Antibody Testing) utaendelea kufanywa na Maabara ya Taifa kwa utaratibu uliokuwepo wa kufika Maabara ya Taifa kuchukuliwa sampuli na kupata cheti cha kipimo hiki kwa wasafiri wanaohitaji kipimo hicho kulingana na mahitaji ya nchi husika wanazokwenda.

Vilevile, kwa wasafiri maalumu wale wanaohitaji kipimo cha haraka cha COVID-19 Antigen wataendelea kupimwa katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere International Airport (JNIA) na Kilimanjaro International Airport (KIA) yakiwa ni matakwa ya ndege zao ambapo watapimwa saa nne kabla ya ndege kuondoka.

Wasafiri wote watatakiwa kwenda kwenye vituo vya kuchukulia sampuli kama ilivyotolewa kwenye Mwongozo wa Ushauri kwa Wasafiri (Travellers Advisory).

Hivyo kuanzia tarehe 01 Machi, 2021 Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii haitapokea wasafiri na kuwachukua sampuli na badala yake itabaki na jukumu la kupima na kutoa vyeti ikiwa ndio jukumu lake la msingi.

**Imetolewa na:**



Gerard Julius Chami

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO YA SERIKALI  
WAMJW - Afya**

*Approximate translation using Google Translate:*

## REMOVING NATIONAL LABORATORIES IN RESPONSIBILITY TO TAKE TRAVEL SAMPLES.

Morogoro, Saturday February 27, 2021.

The National Laboratory has been taking samples, processing and testing them, provide feedback as well as preparation of certificates for travellers. In addition, in carrying out that role, The National Laboratory has been a challenge for overcrowded travellers, leading to overcrowding, as well as overcrowding infrastructure and limited parking.

The Ministry of Health has decided to remove the National Laboratory from the option of providing a COVID-19 sampling centre for travellers in the [pimacovidmoh.go.tz](https://pimacovidmoh.go.tz) dispatch system from 01 March, 2021.

In addition, The process of testing the samples for rapid immunization of immune proteins (COVID-19 IgM Antibody Testing) will continue to be carried out by the National Laboratory for the existing procedure to arrive at the National Laboratory to be sampled and obtain a certificate of this test for travellers who need the test according to need of the respective countries they are going to.

Similarly, for special travellers those who need a rapid test of COVID-19 Antigen will continue to be tested at Julius Nyerere International Airport (JNIA) and Kilimanjaro International Airport (KIA) as a prerequisite for their flights where they will be tested four hours before departure. .

All passengers will be required to go to the sampling centres as provided in the Travelers Advisory Guide.

So starting on 01 March, 2021 The National Public Health Laboratory will not accept travellers and take samples and will instead be responsible for testing and certifying as its primary responsibility.